TAKUKURU MWANZA YAKAGUA MIRADI YA THAMANI YA TSHS BILIONI 27 KATIKA KIPINDI CHA APRILI-JUNI 2022.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (M) Mwanza imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ambapo katika kipindi cha April –Juni,2022 mkazo uliwekwa zaidi katika kazi ya **Uzuiaji Rushwa** kwa kuendelea kukagua miradi ya maendeleo hasa ile inayotekelezwa kwa pesa za UVICO 19, ili kuhakikisha kwamba pesa zinazotolewa kwa ajili ya miradi hiyo zinafikia malengo yaliyokusudiwa.

Katika eneo la **UZUIAJI RUSHWA** na kwa kuzingatia kwamba miradi ya maendeleo ni mali ya wananchi na serikali inapeleka fedha nyingi katika eneo hilo, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza **imefuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ishirini na miwili (22)** yenye **thamani ya Tsh.Bilioni 27(27,368,322,334)** katika sekta ya Elimu, Barabara, Maji, Usafi wa mazingira na Afya. Hii inajumuisha miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Uviko 19 pamoja na miradi inayotekelezwa kwa fedha za tozo (Fedha za ndani)

Ufuatiliaji wa TAKUKURU katika utekelezaji wa Miradi hii ulibaini mapungufu kadhaa katika miradi ya Afya, Maji na Elimu ikiwemo kuchelewa kukamilishwa kwa mujibu wa mkataba kutokana upungufu wa fedha zilizotolewa na serikali, baadhi ya wazabuni kushindwa kuleta vifaa na vifaa tiba kwa wakati, kupanda kwa bei za vifaa ya ujenzi kunakopelekea ongezo la gharama za ujenzi pamoja na manunuzi kufanyika kwa gharama ya juu ya bei ya soko.

Mapungufu husika yalirekebishwa kwa kutoa elimu na kusimamia kufanyika kwa marekebisho kwa kushirikiana na wadau.

Pia TAKUKURU katika Uzuiaji Rushwa hufanya kazi ya Uchambuzi wa Mfumo ili kubaini maeneo yenye mianya ya rushwa katika utoaji wa huduma kwa wananchi na kisha kutoa ushauri wa namna bora ya kuziba mianya hiyo.

Katika kipindi cha April-Juni, TAKUKURU ilifanya uchambuzi wa mfumo katika katika sekta za Ujenzi, Maji na Mikopo inayotolewa na Halmashauri. Mambo mbalimbali yamebainika katika chambuzi hizi za Mifumo ikiwa ni pamoja na ;

- Uwepo wa leseni nyingi na vibali vinavyotolewa kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya ujenzi lakini hakuna maeneo maalum yaliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya uchimbaji huo na
- Pia wakusanya mapato hufanya kazi ya ukusanyaji kwa kuvizia njiani magari yaliyobeba madini ya ujenzi. Utaratibu huu unazinyima Halmashauri mapato yatokanayo na tozo za madini ya ujenzi.
- Katika uchambuzi wa mfumo wa Mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa makundi maalum ya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu, ilibainika kwamba urejeshwaji wa Mikopo hiyo ni mdogo ukilinganisha na muda waliopaswa kufanya marejesho hayo. Mfano mpaka kufikia mwezi June 2022 Fedha iliyokopeshwa kwa makundi 65 ya Wanawake ,Vijana na Watu wenye ulemavu ilikuwa **Tshs 220,888,687.40** na kati ya hizo kiasi kilicho rejeshwa kilikuwa **TShs 110,976,599.80** na kiasi kinachodaiwa kilikuwa **Tshs 109,912,087.60** katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.
- Pia ilibainika kwamba Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake,Vijana na Watu wenye ulemavu ya mwaka 2019 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2021 hazifuatwi jambo linalopelekea ufuatiliaji kutofanyika na kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kwa wakati.

Vile vile katika Kazi ya Uzuiaji Rushwa, vilifanyika vikao kwenye Idara ya Maendeleo ya Jamii ikiwahusisha watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza wanaohusika katika Utoaji na Usimamizi wa Fedha zinazotengwa na Halmashauri kwa ajili ya makundi ya Wanawake,Vijana na watu wenye ulemavu. Pia Kikao cha Warsha kujadili mianya ya rushwa juu ya matumizi ya “force akaunti” kwenye usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kilifanyika ambapo maazimio ya kuziba mianya ya rushwa na upotevu wa fedha za umma yalifikiwa.Vikao hivi vilifanyika ili kujadili na kuweka mikakati ya kuziba mianya ya rushwa na upotevu wa fedha za Serikali katika idara hizo.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kwa upande wa E**LIMU KWA UMMA** katika kipindi cha April-June 2022, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imetoa Elimu kwa lengo la kuyafikia makundi mbalimbali kwa kufanya semina 30, mikutano ya hadhara 17, uandishi wa Makala 11, na maonesho 2.

Pia klabu za wapinga rushwa 106 kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo zimetembelewa na kuimarishwa ambapo kupitia klabu hizi vijana wamekuwa wakielimisha na kukumbushwa masuala ya maadili mema na kukuza kizazi kinachochukia Rushwa na mwamko wa vijana kujiunga na klabu hizi umekuwa mkubwa

Aidha katika kipindi hiki mkazo zaidi wa elimu umetolewa kwa watumishi wa Idara mbalimbali za Serikali kuhusu umuhimu wa uadilifu, uwajibikaji na uhusiano kati ya Uadilifu na Rushwa katika utumishi wa Umma. Vilevile wamekumbushwa kushiriki kuhesabiwa katika zoezi la sensa ya watu na makazi tarehe 23/08/2022.

Lengo la Uelimishaji kwa Umma ni kuwa na uelewa wa pamoja wa mambo mbalimbali yahusuyo kukemea na kuzuia Rushwa katika maeneo yao.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Ingawa zimekuwepo jitihada mbalimbali za Uzuiaji Rushwa na Uelimishaji wa jamii, bado vitendo vya rushwa vimeendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo ambapo katika kipindi cha mwezi Aprili-Juni 2022, jumla ya malalamiko 115 yamepokelewa ambapo taarifa za rushwa zilikuwa 86 na zisizo za rushwa zilikuwa 29.

Taarifa zilizohusu rushwa ziligusa Sekta za TAMISEMI (27), Elimu (7), Afya (5),Polisi (2),Mahakama (1),Ardhi(6) na sekta nyinginezo (38).Taarifa hizi zinazohusu rushwa zimeshughulikiwa kwa muujibu Sheria.

Aidha majalada 10 ya uchunguzi yamekamilika na mashauri 08 mapya yamefunguliwa Mahakamani na kufanya jumla ya mashauri yanayoendelea Mahakamani kufikia 24.Idadi ya Mashauri yaliyoamuliwa katika kipindi hiki ni manne (4) ambapo Jamhuri ilishinda katika mashauri mawili (2).

Taarifa 29 zisizohusu rushwa , walalamikaji walishauriwa mahali sahihi pa kuziwasilisha na wengine walipelekwa taasisi stahiki kwa msaada zaidi ,hivyo taarifa hizo zilifungwa.

Tunapenda kuwakumbusha wananchi kuendelea kutoa taatifa zinazohusu vitendo vya rushwa vinavyoangukia katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007 kwani bado watu wengi wanakuja kutoa taarifa ambazo sio za Vitendo vya rushwa.

Ndugu Waandishi wa Habari,

TAKUKURU Mkoa wa Mwanza inayo mikakati iliyojiwekea katika kipindi cha JULAI – SEPTEMBA 2022 kwa kuzingatia mpango kazi wa Kitaifa.

TAKUKURU Mkoa wa Mwanza inatarajia katika robo hii ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022-2023 Kuendeleza juhudi za Kuzuia Rushwa kwa kukagua miradi ya maendeleo na kuhimiza matumizi sahihi ya fedha zinazoletwa kwa ajili ya utekelezwaji wa miradi hiyo, pamoja na usimamizi sahihi ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa na tutaendelea kuwakumbusha wananchi kushiriki kutoa taarifa za miradi inayotekelezwa chini ya kiwango katika maeneo yao.

TAKUKURU itaendelea kutumia njia mbalimbali za uelimishaji zinazolenga kubadilisha mitizamo ya wananchi dhidi ya rushwa na kuongeza uelewa wao kwa nia ya kujenga uwezo wa kila mwananchi kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini.

Pia TAKUKURU itaendelea kuchambua mifumo ya utendaji kazi wa Taasisi za Umma,za Serikali na Binafsi ili kubaini mianya ya rushwa ndani ya taasisi hizo na tunatarajia kukaa vikao vya Warsha na wadau mbalimbali ili kuweka maazimio yanayolenga katika kupunguza au kuondoa kabisa vitendo vya rushwa vinavyopelekea kukosekana kwa ufanisi wa kiutendaji na utoaji mbaya wa huduma kwa wananchi.

Tunavishukuru vyombo vya habari mkoani Mwanza na tunatambua mchango wao mkubwa katika kutangaza mafanikio ya TAKUKURU katika Kuzuia na Kupambana na Rushwa pamoja na kutoa fursa za Uelimishaji Umma juu ya dhana ya rushwa na madhara yake kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Wito kwa wananchi;

Ninawaomba wananchi wa Mkoa wa Mwanza waendelee kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa na kushiriki katika kutoa ushahidi mahakamani ili hatua stahiki ziweze kuchuliwa kwa wahusika wa vitendo vya rushwa kwa mujibu wa sheria.

Mwisho,

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LANGU

“Kwa taarifa za vitendo vya rushwa tafadhali fika ofisi ya TAKUKURU iliyo karibu nawe au piga simu ya dharura namba 113 au tuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au Piga *113# fuata maelekezo” Huduma hii ni ya BURE.

IMETOLEWA NA:
SIGNED
FRANK MKILANYA - 0738 150 162
MKUU WA TAKUKURU (M) MWANZA